**Learning by Ear 2010 – Urban Exodus**

**Episode 09: "Dark clouds on the horizon"**

**Author: Alfred Dogbé**

**Editor: Yann Durand**

**Translator: Anne Thomas**

WAHUSIKA:

Onyesho la 1:

- **HADARI** (UMRI MIAKA 48, MKUU IDARA YA HUDUMA ZA MASHAMBANI)
- **TINGO** (UMRI MIAKA 32, MKULIMA WA KISASA)

Onyesho la 2:

- **ZEINA** (UMRI MIAKA 24, MCHUMI, RAFIKI YAO BAKI NA BEN)
- **NANA** (UMRI MIAKA 22, KIONGOZI WA CHAMA CHA VIJANA)
- **HADIA** (UMRI WA MIAKA 45, MAMAKE NANA)

Onyesho la 3:

- **BEN** (MHANDISI WA KILIMO, UMRI WA MIAKA 29)
- **KABO** (MKULIMA, MJOMBAKE BEN, UMRI WA MIAKA 57)
- **BAKI** (UMRI MIAKA 26, MWANAELIMUJAMII, RAFIKI YA ZEINA NA BEN)
- **ZEINA** (UMRI WA MIAKA 24, MCHUMI, RAFIKI YA BAKI NA BEN)
- **NANA** (UMRI MIAKA 22, KIONGOZI WA CHAMA CHA VIJANA)

**Intro:**

Karibu kwenye kipindi kingine cha *Learning by Ear*, ambacho ni cha tisa cha mfululizo wa vipindi vyetu unaoitwa “Kukabiliana na Wimbi la Mabadiliko” kuhusu uhamiaji mijini. Tunafuatiliza masaibu ya Ben, Baki na Zeina, vijana watatu wasio na ajira walio na shahada za chuo kikuu ambao wameamua kuondoka mjini kuelekea kijijini kwao kuanzisha chama cha ushirika cha ukulima. eo tutagundua kwamba si watu wote wanaofurahishwa na ufanisi wa chama hicho cha ushirika. Chama hicho kina mpinzani mmoja mkuu:

**Scene 1: Hadari's office.**

**HADARI, TINGO**

1. **ATMO: OFFICE SOUNDS. COMPUTER KEYBOARD, TELEPHONE RINGING, SNIPPETS OF CONVERSATION IN THE BACKGROUND**

2. **TINGO** Bwana Hadari...

3. **HADARI** Bwana Tingo...! Nikusaidie vipi?

4. **TINGO** Kwa kawaida, kila mara ninapokuhitaji, mimi hukuletea ujumbe uje shambani kwangu lakini leo nina jambo la dharura!

5. **HADARI** Dharura?

6. **TINGO** Ndio! Lakini kwanza, ebu nambie… je, ni kweli kwamba umewaambia wale vijana wahuni wawasilishe maombi ya msaada wa kifedha?

| | | |
|---|---|---|
| **7.** | **HADARI** | Ni jukumu langu kutoa habari kwa yeyote anayehitaji. Kama wataka, basi umechelewa! |
| **8.** | **TINGO** | Lazima uzuie barua yao ya maombi! |
| **9.** | **HADARI** | Nimeshawasilisha nyaraka zao za kujisajili. Wala si barua moja tu bali ni barua tatu za maombi. Wanaweza kuomba aina tatu za ufadhili wa kifedha. Fungu la kwanza ni la kurutubisha udongo, la pili la ununuzi wa miche bora na la tatu... |
| **10.** | **TINGO** | Hivi kwani wewe na wao mmekula njama ya kunimaliza? |
| **11.** | **HADARI** | Hata kidogo! Hawajapanga kushindana nawe – hawataki kujishughulisha na kilimo cha njugu. |
| **12.** | **TINGO** | Kwani wewe mpumbavu nini? Hawatashindana nami kwa kile ninachokuza lakini kwa wale wanaonisaidia kukikuza. Hakuna mtu atakayekubali tena kunifanyia kazi! |
| **13.** | **HADARI** | Usijali. Hawataki kumwajiri mtu, kama wewe ufanyavyo. Mwanakijiji yeyote atakayeamua kushirikiana nao atakuwa anabahatisha na hilo si jambo rahisi. Hutakosa watu watakaokubali kukufanyia kazi shambani mwako. |
| **14.** | **TINGO** | Unayosema si mapya. Lakini yaelekea huna habari kwamba hatua yao hiyo itavuruga mambo mengi – itasababisha kiwango cha ujira tunaolipa kipande. Hili ni pigo kubwa kwangu! |
| **15.** | **HADARI** | Kweli unayosema! Lakini wataka nifanyeje? |

**16.** **TINGO** Hadari, lazima usitishe jambo hilo. Nakuahidi hutojuta! Sikiza, waache wapelekee barua za maombi lakini utakapoziwasilisha hakikisha kwamba hati moja au mbili muhimu hazipo…

**17.** **HADARI** Kusema kweli, hilo haliwezekani!

**18.** **TINGO** Nachokuomba ni kuondoa baadhi ya nyaraka tu… au unawaweza kuziwasilisha zikiwa katika utaratibu usiofaa. Yaani faili moja likiwa na nyaraka pungufu na lingine likiwa na nyaraka zisizofaa… Unanifahamu?

**19.** **HADARI** Hapana!

**20.** **TINGO** Aarghhh! Jambo jepesi hivyo! Nisikize rafiki yangu mpendwa Hadari, ukifanya hivyo, utaiona hisani yangu… Maisha yako ya usoni yatanyooka… (**Long silent pause**) … Kwani huna la kusema?

**21.** **HADARI** Siwezi kufanya hivyo! Vijana hawa wanafanya jambo nililopaswa kuliendeleza tangu miaka kumi iliyopita… Siwezi kuutilia guu mradi wao. Unafahamu? Ni kama kwamba wananisaidia kusahihisha makosa niliyoyatenda...

**22.** **TINGO** Sawa! Naona umeshapata washirika wapya. Ni haki yako hiyo. Lakini tahadhari! Nitawaangamiza ninyi nyote. Nitahakikisha chama chenu kimepigwa marufuku. Na ukibahatika, utaishia kuwa ombaomba! Wala sisemi uongo!

**23.** **SFX: FURIOUS STEPS GOING AWAY, THE DOOR OPENS**

**24. HADARI** Bwana Tingo! ... Bwana Tingo...

**25. SFX: DOOR SLAMMING VIOLENTLY**

**----- MUSIC -----**

**Scene 2: At Nana's.**

**HADIA, NANA AND ZEINA**

**26. ATMO: KITCHEN NOISES, HENS**

**27. HADIA** Alaa, nani huyu? Zeina umetutembelea?

**28. ZEINA** Ndiyo, shangazi! Nimekuja kukuona.

**29. HADIA** Kwanza, unieleze kwa nini umeamua kunitembelea leo! Nana, kwani kuna nini?

**30. NANA** Hakuna! Zeina amekuja kukuamkia tu.

**31. HADIA** Ni kuhusu hali ya afya ya Baki?

**32. ZEINA** Hapana! Baki ashaondoka hospitalini. Hata ameshaanza tena kufanya kazi.

**33. HADIA** Basi… Nambieni ukweli mara moja! Ninahisi kama kwamba kuna shida… tatizo na wanaume, siyo?

**34. NANA** Hapana, unachukulia mambo visivyo! Kama kawaida yako!

**35. HADIA** Sema utakavyo! Lakini hujanambia lolote kuhusu chakula. Je alikipenda?

| | | |
|---|---|---|
| **36.** | **NANA** | Naam, alikipenda sana. |
| **37.** | **HADIA** | Alisema nini? Niambie! Zeina, dada yako huyu huweka siri mambo yake. Nadhani hata pengine hajakuambia kuhusu chakula alichompelekea mpenzi wake… |
| **38.** | **ZEINA** | Nana ameniambia kwamba ulipika chakula. |
| **39.** | **HADIA** | Aha ha! Unajua hilo? |
| **40.** | **ZEINA** | Bila shaka! Nana hanifichi jambo lolote. Hata Ben mwenyewe pia. |
| **41.** | **HADIA** | Ben? Ana nini huyu Ben? |
| **42.** | **ZEINA** | Nachanganyikiwa. Nana hakukwambia kwamba chakula kilikuwa cha Ben? |
| **43.** | **NANA** | Ben amekushukuru sana kwa kumjali, ma. Amependezwa na chakula hicho! |
| **44.** | **ZEINA** | Ukweli ni kwamba Nana hawezi kukufikia kwenye mambo ya upishi. |
| **45.** | **HADIA** | Alaa, kwa hivyo Ben ndiye mwenye bahati? |
| **46.** | **ZEINA** | Una maana gani? Kwani nani mwingine? Nachanganyikiwa. Mbona hunambii kwamba una mwengine humu kijijini? |
| **47.** | **NANA** | Hapana. |
| **48.** | **ZEINA** | Nahisi kama kwamba kuna jambo hutaki kunambia… |

**49. NANA** Hakuna! Nakuapia hakuna.

**50. HADIA** Sasa tueleweje?

**51. NANA** Nani ajuaye?

**52. HADIA** Zeina mwanangu, pita ukae. Kiti hiki hapa! Haya, na wewe una habari gani?

**53. NANA** Ataolewa na Baki. Amekuja kukuomba umsimamie arusi yake.

**54. HADIA** Bila shaka! Sikuitwa mpatanishi kiholela. Nimefurahi sana. Hii ni heshima kubwa kwangu kwa kweli!

**55. ZEINA** Asante sana! Nani ajuaye, huenda arusi yangu ikawavutia wasichana wengineo wakubwa hapa kijijini nao kutaka kuolewa.

**56. HADIA** Mungu ajalie iwe hivyo. Mwalike aje hapa nyumbani na umwambie chakula hapa kitakuwa kitamu zaidi.

**57. NANA** Nani? Baki?

**58. HADIA** Hapana! Ben!

**---- MUSIC -----**

**Scene 3: At Ben's. Late at night.**

**BEN, BAKI, ZEINA, NANA, KABO**

**59. ATMO : CRICKETS, NIGHT BIRDS, FROGS**

**60. BEN** Kuna tatizo hapa, kuna tofauti kati ya matatizo tunayokabiliana nayo na faida tunayotaraji.

**61. ZEINA** Acha kukosoa kazi za wenzako! Tumetumia muda wa wiki mbili kushughulikia nyaraka hizo za maombi.

**62. BAKI** Ndiyo hivyo! Hiyo ni sababu tosha yetu sisi kuwa makini tunapozishughulikia nyaraka hizo!

**63. ZEINA** Baki! Kila mara, unatuambia tumesahau hiki hatujafanya hivi!

**64. BAKI** Ni kawaida hiyo! Sijashiriki katika mchakato huu wa kuwasilisha maombi ili niweze kubaini matatizo. Hivyo tu!

**65. KABO** Hata hivyo, unaonekana kufurahia usemayo!

**66. BAKI** Sijadhamiria kuwaudhi, kwa mfano, tumedokeza kwamba wanakijiji hawana elimu ya kutosha na hawafahamu zaidi kuhusiana na mfumo wa vyama vya ushirika. Hata hivyo, hatujatafuta njia ya kulishughulikia suala hilo.

**67. NANA** Basi, inatubidi tuzingatie mantiki ya maombi yenyewe tangu mwanzo.

**68. ZEINA** Vyama vyote vya ushirika vinapaswa kuwaelimisha wanachama wake kuhusu taratibu za kuungana na kushirikiana. Hiyo ni hatua muhimu ili wanachama wa chama cha ushirika washirikiane kwa dhati huku wakijibidiisha kuafikia malengo yao.

| | | |
|---|---|---|
| **69.** | **BEN** | Kwani lazima hayo masuala yajumuishwe kwenye mradi? |
| **70.** | **BAKI** | Ndiyo! Ni jambo la msingi. Tunapaswa kuandaa mradi utakaowafunza watu jinsi ya kushirikiana. Mradi huo pia ni lazima uzingatie hali halisi ya maisha kijijini mwetu pamoja na malengo yetu sisi waasisi. |
| **71.** | **ZEINA** | Basi inaonekana tutahitaji fedha nyingi. |
| **72.** | **BAKI** | Si hoja gharama za mradi wetu lakini tuzingatie manufaa ya mradi wenyewe. Baadaye tunaweza kuuangalia upya mradi kwa lengo la kupunguza gharama. |
| **73.** | **KABO** | Wanangu, najisikia mchovu. Siwezi tena – afadhali tumalize yaliyobaki kesho! |
| **74.** | **ZEINA** | Itatubidi pia kuangalia upya makadirio yetu ya fedha kwa sababu... |
| **75.** | **KABO** | Nisikizeni, tumekuwa hapa tangu asubuhi. Naomba tuachie hapa tafadhali! Mimi hapa nilipo nimeshakuwa mtu mzima! |
| **76.** | **NANA** | Nakubaliana nawe – tuachieni hapa. |
| **77.** | **BAKI** | Tuna muda wa siku mbili kabla ya kuwasilisha maombi. |
| **78.** | **BEN** | Sawa, tuachieni hapa! |
| **79.** | **KABO** | Lakini kabla hatujaondoka, ningependa kusema kwamba yote haya tumeyapata dhamana na Hadari. Yeye ni binadamu mwenye ila zake lakini ametusaidia sana kwa kweli. Tunapaswa kumshukuru! |

**80.** **BAKI** Unapendekeza nini?

**81.** **NANA** Sasa ndio tumeshaingilia mada nyingine – mazungumzo yasiyokwisha.

**82.** **KABO** Sivyo! Nimewatanabahisha tu. Ebu tulifikirie hilo ili baadaye tuamue la kutenda. Bora sasa tuvunje kikao!

**83.** **BAKI** Je, mna habari kwamba kiwango cha mavuno ya njugu kimeshuka kwa kiasi kikubwa?

**84.** **NANA** Hilo litamtatiza Tingo!

**85.** **BEN** Hata na wanakijiji. Zaidi ya theluthi mbili ya mapato ya kijijini hutokana na ujira wa kumfanyia kazi Tingo.

**86.** **BAKI** Hata kama ni malipo duni!

**87.** **ZEINA** Ni malipo duni lakini jambo hili ni pigo kubwa kwa watu, na athari zake ni kubwa.

**88.** **NANA** Wakati mwingine shari huja kuwa heri… Wanakijiji wataelewa mambo ambayo tumekuwa tukiwashauri siku nenda siku rudi! Ni njia mwafaka ya kutangaza malengo yetu!

**89.** **BAKI** Nilipozisikia habari hizo redioni nilicheka sana, lakini hili si jambo la kuchekesha!

**90. BEN** Itategemea na jinsi atakavyokabiliana na hali hiyo. Ikiwa anachotaka tu ni kuhifadhi fedha zake, basi atapata pigo kubwa. Vinginevyo hii ni njia mwafaka ya kuimarisha shughuli za kilimo katika eneo hili.

**91. BAKI** Yule bwana ni nyoka.

**92. ZEINA** Usimdharau maana hatakosa la kutenda.

**93. BEN** Kama hali hii itamtanabahisha, huenda akawa mshirika wetu muhimu.

**94. NANA** Ben, una maana kwamba ungependa kushirikiana na huyo bwana?

**95. BEN** Mbona nisishirikiane naye? Ilimradi tutafuata malengo yetu na tuwe huru, tunaweza kushirikiana na mtu yeyote.

**96. NANA** Ati?

**97. BAKI** Usiwe na wasiwasi Nana! Sidhani kama huyo bwana atabadilika hivi karibuni na kuwa na roho ya binadamu!

**98. SFX: GENERAL LAUGHTER**

**99. KABO** Hapa mimi nasinzia! Kwaherini!

**100. EVERYONE** Kwaheri! Kwaheri! Mjomba Kabo!

**101. BEN** Tukutane tena kesho saa tatu kamili asubuhi. Nyaraka nabaki nazo mimi...

**102. NANA** Wabaki nazo za nini?

**103. BEN** Nataka kuzipitia kwa mara nyingine...

**104. NANA** Hapana! Tumesema tutaachia hapa. Maanake kila mtu! Uliniahidi tutaandamana nyumbani. Mamangu anatusubiri!

**105. KABO** Ben, mwanangu! Maisha si kazi tu! Penye kazi pana kupumzika!

**106. BAKI** Kazi yenyewe ndiyo maisha…

**<u>Outro:</u>**

Huo ndio mwisho wa kipindi cha *Learning by Ear* hivi leo. Ni kipindi cha tisa cha mfululizo wa vipindi vyetu kuhusu uhamiaji mijini.

Usikose kusikiliza kipindi chetu cha mwisho ili ujue iwapo Tingo atakabiliana na Ben pamoja na marafiki zake.

Kama ungetaka kukisikiliza tena kipindi hiki au kutupatia maoni yoyote, fungua ukurasa wetu wa tovuti dw-world.de/LBE au utuandikie barua-pepe kupitia anwani yetu lbe@dw-world.de.

Usikose kusikiliza kipindi kijacho!

**END OF EPISODE 9**